

Ruhusa ya jumla ya kuchapisha na kufichua taarifa

Mpendwa Mzazi/Mlezi

Naomba ruhusa yako kuruhusu shule/Idara ya Elimu ili kuchapisha na/au kufichua habari kuhusu mtoto wako kwa madhumuni ya kushiriki uzoefu wake na wanafunzi wengine, kufahamisha shule na jamii kubwa kuhusu shughuli za shule na za wanafunzi na kurekodi ushiriki wa wanafunzi katika miradi muhimu au huduma ya jamii.

Habari hii inaweza kujumuisha jina la mtoto wako, umri, darasa lake na taarifa inayokusanywa shuleni kama vile picha, rekodi za sauti na za kuona za mtoto wako, kazi ya mtoto wako na maoni yake kama vile katika vyombo vya habari vinavyoingiliana.

Mawasiliano ambayo taarifa ya mtoto wako yanaweza kuchapishwa au kufichuliwa yanajumuisha lakini hayazuiliwi:

- Tovuti za umma za Idara ya Elimu ikijumuisha tovuti ya shule, intraneti ya Idara ya Elimu (wafanyakazi pekee), blogu na wiki
- Machapisho ya Idara ya Elimu ikijumuisha jarida la shule, jarida la kila mwaka la shule na ripoti ya shule, nyenzo za utangazaji zilizochapishwa kwa njia za uchapishaji na kielektroniki ikijumuisha kwenye tovuti za Idara
- Akaunti rasmi za mitandao ya kijamii za Idara na shule kwenye mitandao kama vile YouTube, Facebook na Twitter
- Magazeti ya mtaa na miji mikuu na majarida na vyombo vingine vya habari.

Wazazi wanapaswa kufahamu kwamba taarifa inapochapishwa kwenye tovuti za umma na chaneli za mitandao ya kijamii, inaweza kutambulika mtandaoni kwa miaka kadhaa, ikiwa sivyo kabisa. Mitambo ya utafutaji inaweza pia kuweka akiba au kuhifadhi nakala za taarifa zilizochapishwa. Taarifa zilizochapishwa pia zinaweza kuunganishwa na wahusika wengine.

Tafadhali ujaze fomu ya ruhusa na uirudishe shuleni kufikia tarehe inayofuata:

Date for return of permission form

Usaidizi wa mkalimani

Ikiwa ungependa habari zaidi tafadhali wasiliana na shule.

Ikiwa unahitaji usaidizi wa mkalimani kuwasiliana na shule, upige simu 131 450, umwambie mwendeshaji wa simu lugha unayohitaji na umwulize kupiga simu kwenye shule. Mpigiaji simu atapata mkalimani kwenye simu kukusaidia kwa mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hiyo.

Mwaminifu wako

Jina la mkuu wa shule (Name of principal)

Jina la shule (Name of school)

education.nsw.gov.au

Ruhusa ya mzazi/mlezi ya kuchapisha ruhusa Parent/carer permission to publish consent

Nimesoma ruhusa hii ya kuchapisha na:

(Weka alama kwenye kisanduku kimoja tu hapa chini na uache kingine kikiwa wazi)

Natoa ruhusa kwa shule/Idara ya Elimu kuchapisha taarifa kuhusu mtoto wangu kama ilivyoelezwa hapa juu, ikiwa ni pamoja na mawasiliano ya kupatikana kwa umma.

I give permission to the school/Department of Education to publish information about my child as described above, including in publicly accessible communications.

Sitoi ruhusa kwa shule/Idara ya Elimu kuchapisha taarifa kuhusu mtoto wangu kama ilivyoelezwa hapa juu, ikiwa ni pamoja na mawasiliano ya kupatikana kwa umma.

I do not give permission to the school/Department of Education to publish information about my child as described above, including in publicly accessible communications.

Ruhusa hii iliyotiwa saina itaendelea kutumika hadi niishauri shule vinginevyo.

Jina la mtoto (tafadhali uandike)

Name of child

Jina la mzazi/mlezi (tafadhali uandike)

Name of parent/carer

Saini ya mzazi/mlezi

Signature of parent/carer

Tarehe

Date